

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 30261
Kibaha, Pwani.
Nukushi: (023) 2402657
Barua pepe: rbcpwani@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

PWANI-FEBRUARI 23, 2021

**MIMBA KWA MWANAFUNZI YAWA MWIBA KWA MWANANCHI NA
KUANGUKIA MIKONONI MWA TAKUKURU**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wilaya ya kibiti mkoani Pwani imemfikisha Mahakamani mwananchi aitwaye **RASHID HAMIS MTOLEA** katika Mahakama ya Wilaya ya Kibiti kwa makosa ya kushawishi na kutoa rushwa ya Sh. 250,000/= (Shilingi laki mbili na elfu hamsini) kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Awali Mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa kushawishi na kutoa Rushwa kwa Afisa elimu kata ya Mlanzi **Bw. IDD SALIMU ALLI** ili asimchukulie hatua za kisheria kwa kutompeleka mtoto shule kwa ajili ya kujiunga kidato cha kwanza kwa madai kwamba mtoto huyo ni mjamzito.

Hata hivyo mshitakiwa alikiri makosa yote mawili mbele ya mahakama na hivyo kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu au kulipa faini ya shilingi laki Tano (Sh. 500,000/=) kwa makosa yote mawili ambapo mtuhumiwa aliamua kulipa faini.

WITO WA TAKUKURU KWA WANANCHI

Nitumie fursa hii kuwaasa wananchi wa mkoa wa Pwani kuendelea kutoa taarifa katika ofisi zetu ili tuweze kuwachukulia hatua wananchi waliozoea kuwashawishi watumishi wa umma ili wasitekeleze majukumu yao. Mtumishi huyu aliyetoa taarifa za kushawishiwa ni mfano wa kuigwa na ni vyema na watumishi wengine mkaiga mfano huu.

Kwa pamoja tuseme SASA RUSHWA BASI

Asanteni kwa kunisikiliza!

I metolewa na:

Suzana Raymond-0738 150176

MKUU WA TAKUKURU (M)

PWANI